
TaCRI
TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA

TaCRI inachangia katika kuboresha Tasnia ya Kahawa Tanzania



Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) ilisajiliwa rasmi mwaka 2000 ikiwa na lengo la kuchangia katika kuboresha tasnia ya kahawa Tanzania iwe na ustawi endelevu. Makao makuu ya Taasisi yako Lyamungu chini ya miteremko ya rutuba nzuri ya mlima Kilimanjaro. Taasisi inaendesha vituo vingine vidogo vinavyosaidia utafiti wa kahawa kwenye kanda zote muhimu zinazolima kahawa.

Jukumu kuu la TaCRI ni kuendeleza na kueneza teknolojia mwafaka ili kuinua tija ya kahawa ndani ya muundo mzuri wa sera na kupunguza gharama za uzalishaji.

Matokeo tarajiwa ni kuongeza ushindani wa kahawa za Tanzania katika soko la dunia na hatimaye kuongeza kipato, kupunguza umasikini na kuboresha maisha ya wazalishaji wadogo wa kahawa 400,000 na mashamba makubwa 110.

Historia ya kahawa

Zao la kahawa limekuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania tangu kahawa iingizwe nchini takribani miaka 100 iliyopita.

Lakini tasnia imekuwa kwenye hali ya maporomoko kuanzia miaka ya 1990. Hii inatokana na sababu tofauti: mporomoko wa bei kwenye soko la dunia umepunguza kipato na faida kwa wazalishaji; ikitishia maisha; hii imechangia katika kupunguza ari na imani ya wazalishaji katika kuwekeza kwenye pembejeo na kilimo bora; gharama kubwa za uzalishaji zinapunguza ushindani kwenye soko la dunia; aina za kahawa za sasa zinashambuliwa na magonjwa; miti ya kahawa na wakulima wenyewe wamezeeka. Hali ni mbaya!



Mustakabali wa matumaini

Baada ya kusema hayo, mipanuko ya maeneo ya miinuko ya volkeno na bonde la Ziwa Victoria ni mazingira mazuri sana kwa kuzalisha kahawa bora kuliko zote ulimwenguni – kahawa bora zitakazopata bei nzuri za kuaminika zaidi kwenye soko la dunia.

Uwezo ni mkubwa – uwezo ambao unafunguliwa na TaCRI sasa kwa utafiti imara unaokidhi mahitaji ya wadau, utafiti ambao ni muhimu sana ili kuwa na tasnia yenye msisimko.

Kusarifika

Mapato ya TaCRI yanatoka kwenye vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivi ni pamoja na ushuru kutoka kwenye mauzo ya kahawa kama mchango wa wazalishaji; michango ya serikali; ushirikiano na taasisi nyingine; na mauzo ya vifaa na huduma mbalimbali. Taasisi imepokea msaada mkubwa kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), msaada ambao ni, na utaendelea kuwa, kichocheo katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za TaCRI. TaCRI itaendelea kufaidika na riba kutokana na sehemu ya fedha hizi zitakazowekezwa kwenye hisa maalum kwa kipindi cha miaka 15 ijayo.

TaCRI imetengeneza muundo wa utafiti endelevu wa kimatend unaolenga mahitaji ya wadau. M sehemu maalum

Uboreshaji wa Zao

Majukumu ya idara hii ni pamoja na kutafiti aina bora za kahawa zinazozaa kwa wingi (Arabica na Robusta) zinazovumilia magonjwa, ambazo pia zina punje kubwa na muonjo mzuri. Idara imetoa aina bora chotara aina za Arabika ambazo zitasambazwa kwa wakulima wa kahawa nchi nzima kupitia uzalishaji wa vikonyo (clonal multiplication) na njia ya chupa (tissue culture).

Huu ni mpango kabambe wa kukarabati mashamba ya zamani na mpango wa upanuzi katika mashamba mapya kwa nia ya kubadilisha miti ya aina za zamani inayokisiwa kufikia milioni 200 nchi nzima.

TaC

TAASISI YA UTAFITI W

Tija na Usindikaji wa Mwanzo wa Zao

Lengo la utafiti katika idara hii ni kutafuta mbinu bora za utunzaji na udhibiti husishi wa visumbufu vya zao ambazo zitakidhi matakwa mbalimbali na matatizo ya mifumo tofauti ya kilimo cha kahawa Tanzania. Matokeo ya utafiti wa idara hii yatasaidia katika kuongeza uzalishaji kwa eneo au kwa mti, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ubora wa kahawa za Tanzania.

Usambazaji Teknol

Idara hii ina wajibu mkubwa TaCRI wa kutangaza matokeo ya utafiti wa Taasisi, na hususan, kutayarisha na kusambaza matokeo ya utafiti wa kahawa kwa wadau wote na tasnia ya kahawa kwa ujumla.

Idara itakuwa na jukumu kubwa muhimu la kuzalisha na kusambaza kwa wingi aina mpya bora za kahawa kwa wakulima wote w sambamba na kutoa mafunzo kwa wakul kwenye bustani zao ikiwa ni pamoja na

utekelezaji wa muda mrefu wa
na mkakati wa utekelezaji
kakati umegawanywa kwenye
tano za utafiti:

KAHAWA TANZANIA

Virutubisho vya Zao

Lengo la idara hii ni kutatua tatizo la kupungua kwa rutuba ya udongo linaloambatana na gharama kubwa ya mbolea za viwandani au upatikanaji wa mbolea za asili. Idara inajihusisha na kutafiti mbinu husishi za kudhibiti virutubisho vya udongo ambazo zitasaidia wakulima kufanya maamuzi sahihi ya gharama nafuu kuhusu mbinu mbalimbali za kudhibiti rutuba ya udongo.



ojia na Mafunzo

kahawa nchini. Kazi hii itakwenda na watakaozalisha miche ya vikonyo uwapa vijitabu vya kiada.

Riziki na Uhakika wa Kipato

Kuna ufahamu mdogo sana unaojulikana kuhusu sababu ambazo zinachangia katika uendelevu na mafanikio ya mifumo inayotofautiana ya kilimo na riziki kwa wakulima wadogo 400,000. Mkazo hapa ni kuelewa zaidi mazingira ambayo wanaishi na kufanya kazi hawa wazalishaji wadogo, kuelewa mifumo ya ukulima na riziki katika maeneo yanayozalisha kahawa nchini, kuweka vipaumbele katika vikwazo vya tija na faida na kupendekeza, kutathmini na kuendeleza suluhisho zinazowezekana.

UCHUNGUZI KIFANI JUU YA UTAFITI WA ZAO LA KAHAWA

Changamoto juu ya uzalishaji miche ya aina mpya za kahawa kwa wingi.

Moja ya malengo muhimu sana ya TaCRI ni kuzalisha na kusambaza kwa wingi aina hizi mpya ambazo zinastahimili magonjwa, zinazaa kwa wingi na zenye muonjo mzuri. Hatima ya lengo hili ni kubadilisha mibuni yote ya zamani inayokisiwa kama million 200 kwa kupanda aina hizi bora mpya.

Huu ni mchakato mrefu na Taasisi inatumia njia zifuatazo kukabiliana na changamoto hiyo

Uchaguzi wa aina mpya za kahawa (chotara)

Kwanza, TaCRI inafanya kazi ya kubaini aina mahsusi za kahawa zinazostahimili magonjwa, zinazaa kwa wingi, zina punje nene (kubwa) na zina muonjo mzuri. Kazi hii inahusisha majaribio ya shambani kwa zile aina ambazo zimechaguliwa na pia majaribio katika kituo cha Utafiti cha Lyamungu ili kuweza kutathmini mafanikio ya aina hizi mpya ukilinganisha na aina za zamani zilizoko kwa wakulima.

Uzalishaji kwa wingi wa aina hizi mpya za kahawa

Mara tu baada ya kubaini aina bora (aina nyingi sasa zimeshatolewa), kazi muhimu ambayo inayobaki ni uzalishaji na usambazaji kwa wingi wa miche kwa wakulima wa kahawa.

Kuzalisha miche kwa njia ya chupa

Njia ya haraka ya kuzalisha miche kwa wingi ni njia ya chupa. Ni njia ambayo inazalisha miche yenye tabia kama za wazazi (chotara) kwa kutumia majani yaliyochukuliwa toka kwa mti mama uliochaguliwa. Faida kubwa ya njia hii ni kwamba inasaidia kuzalisha miche maelfu kwa maelfu toka kwenye mti mama mmoja. Kwa sasa hakuna nyenzo za kuzalisha miche kwa njia ya chupa Tanzania na TaCRI inafanya kazi kwa karibu sana na CIRAD, taasisi ya Kifaransa ya utafiti na wataalam bingwa wa uzalishaji kahawa kwa njia ya chupa, kuona uwezekano wa kuwa na nyenzo za kuzalisha miche kwa njia ya chupa Tanzania.

Uzalishaji wa miche kwa njia ya vikonyo

Kwa wakati huu, uzalishaji wa miche kwa njia ya vikonyo ndiyo inayotumika. Hekta moja ya miti mama imeanzishwa Lyamungu ambayo ina miti 10,000. Miti hii mama ni ile iliyochaguliwa ambayo ni bora zaidi katika kustahimili magonjwa, kuzaa kwa wingi na zenye muonjo mzuri. Machipukizi toka miti mama huvunwa na huandaliwa vikonyo ambavyo hupandwa katika masanduku ya kuchipulia. Vikonyo vyenye mizizi hupandwa kwenye viriba na kutunzwa kabla ya kusambazwa kwa wakulima. Bustani hii ina uwezo wa kuzalisha miche mama 500,000 kwa mwaka.

Ili kuharakisha mpango wa kubadilisha miti ya zamani, imepangwa kwamba vikundi vya wakulima wa kahawa nchi nzima watapata miche toka TaCRI na kuanzisha bustani mama ili waweze kujizalishia miche yao ya vikonyo. Lengo ikiwa ni kuzalisha miche million 5 au zaidi kwa mwaka kwa ajili ya kupanda mashambani ifikapo mwaka 2007.

Kipaumbele cha kwanza

Kuzalisha na kusambaza aina hizi bora mpya za kahawa ndio mafanikio muhimu ya kufikia lengo la TaCRI la kuboresha tasnia ya kahawa nchini. Bodi ya Wakurugenzi ya TaCRI imeamua kwamba uzalishaji na usambazaji wa haraka wa miche ni kipaumbele cha kwanza kabisa cha Taasisi hii.

Kahawa Tanzania inalimwa kwenye maeneo yanayotofautiana kijiografia, hali ya hewa na mifumo ya kilimo. TaCRI ina vituo vidogo kwenye maeneo haya muhimu nchi nzima. Vituo hivi vidogo sio tu vinatumika kutoa mafunzo na usambazaji wa taarifa mwafaka kwa wakulima wa maeneo haya bali pia kama vituo vya utafiti kuainisha teknolojia halisi kwa kila eneo linalolimwa kahawa.

Ramani inayoonyesha maeneo yanayolimwa
kahawa Tanzania na vituo vya TaCRI vya utafiti wa kahawa

Taarifa hii imeandaliwa kwa msaada wa Jumuiya ya Ulaya. Maoni yaliyoelezwa humu ni ya Taasisi Ya Utafiti Wa Kahawa nchini Tanzania na siyo lazima yaakisi maoni ya Jumuiya ya Ulaya.

TaCRI
TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA

TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA
LYAMUNGU
S.L.P. 3004, Moshi, Tanzania.
Simu / Fax: +255 27 2756773, Barua pepe: tacriced@kicheko.com